

HALMASHAURI YA MJI KASULU

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

SimuNa. +255 28 2810355

Website: www.kasulutc.go.tz

Email: td@kasulutc.go.tz



S.L.P 475

KASULU

09/03/2023

KUMB NA. KSTC/S.1/20/110

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kasulu anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na uwezo kutuma maombi ya nafasi ya kazi ya Msimamizi wa Ujenzi (Clerk of Works) kwaajili ya Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi na Marekebisho kwa watu wenye Ulemavu kwa kuzingatia sifa, vigezo na maelekezo yaliyo katika tangazo hili.

1. **Msimamizi wa Ujenzi (Clerk of Works) (Nafasi 1).**

Sifa za Mwombaji.

- i. Awe na cheti cha Kidato cha Nne na Sita
- ii. Awe na Shahada ya Uhandisi kutoka vyuo vikuu vinavyotambuliwa na serikali
- iii. Awe amesajiliwa na Bodi ya usajili ya Wahandisi
- iv. Awe na Cheti cha Professional Engineer.
- v. Awe na uzoefu wa kufanya kazi za usimamizi wa Miradi kwa zaidi ya miaka mitatu (3)

Kazi za Kufanya:-

1. Kusimamia utekelezaji wa mradi
2. Kuandaa makadirio ya gharama za ujenzi kwenye mradi
3. Kupitia mapendekezo ya mradi wa majengo
4. Kutoa ushauri wa kitaalamu na usimamizi wa kazi za ujenzi wa mradi
5. Kufanya ukaguzi wa majengo ya mradi kubaini ubora
6. Kufuatilia utekelezaji wa sheria na kanuni za ujenzi wa majengo
7. Kutayarisha taarifa za maendeleo ya mradi

Masharti ya kazi.

Kazi ina masharti ya Mkatoba

MAMBO YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI.

1. Muombaji awe Raia wa Tanzania
2. Awe mwenye umri kati ya miaka 18 -45.
3. Barua za muombaji ziambatishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma ,Cheti cha Kuzaliwa na Picha mbili(2) za rangi (Passport size) za hivi karibuni.
4. Maomba ya kazi yaambatishwe na nakala ya kitambulisho cha nida au namba ya nida.
5. Barua za maombi ziambatishwe na maelezo binafsi ya muombaji (CV).
6. Testimonials, "Provisional Results" Statement of Results" hati za matokeo za kidato cha Nne na sita (Form IV and Form VI Results Slips) **HAVITAKUBALIWA.**
7. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA)

Namna ya Kuwasilisha maombi:-

- (i) Barua ya maombi iandikwe kwa mkono na iambatishwe passport size.
- (ii) **Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20/03/2023 saa 9:30 Alasiri**

Maombi yote yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji,
S.L.P 475
KASULU.



Dollar R. Kusenge
Mkurugenzi wa Mji
Halmashauri ya Mji
KASULU

